Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Saqifa

Kwanza, ni vizuri kujua maana ya neno: Saqifa: Ni Klabu au ukumbi.

Amesema Mwana Aisha kuwa: "Zilipotangazwa habari za kifo cha Mtume (s.a.w.) Umar bin Khattab na Mughira bin Shuubam waliingia ndani alikolazwa Mtume (s.a.w.). Umar akasema: Oh! msiba mzito kwa kuondokewa na Mtume, kisha walitoka nje, walipokuwa mlangoni Mughira akasema: "Ewe Umar! Kwa kweli Mtume amekufa", Umar akajibu: "Wewe muongo, Mtume hajafa isipokuwa wewe ni mtu unayesumbuliwa na fitina. Mtume hatakufa mpaka wanafiki wamalizike wote."

Taz: Albidayatu Wannihaya J.5 Uk. 212

Hatimae Umar alikamata upanga akaonya kuwa: Ye yote atakaesema kuwa Mtume amekufa atakata kichwa chake. Alipofika Abubakr, Umar akanyamaza na akaweka upanga wake chini. Kisha Abubakr akatangaza kuwa Mtume amekufa, na hapo ndipo alipoondoka yeye na Umar kwenda kwenye ukumbi wa Bani Saida. Huko walijumuika na Masahaba kutoka Ansar wa Madina tayari kwa uchaguzi. Abubakr alitoa hutuba ndefu katika mkutano huo akiwakumbusha kuwa wao (Muhajir) ndio wenye haki ya kushika uongozi mahala pa Mtume (s.a.w.). Hutuba ambayo ilijibiwa baadae na Hubab bin Mundhir katika Ansar, naye akionyesha kuwa ma-Ansar wanayo haki zaidi yao, kwa sababu kwao (Madina) ndiko kuliko shamiri na kukomaa nguvu za Uislam, na Waislamu kupata Uhuru wa kuabudu. na ikiwa hapana budi basi kwa Muhajir atoke mmoja na kwa Ansar atoke mmoja.

Hapo ndipo Umar aliposimama akasema: "Hilo haliwezekani, panga mbili hazikai katika ala moja, Wallahi Waarabu hawakubali kuwatawalisheni na hali Mtume wao hatokani na nyinyi."

Baada ya mabishano makali na kushutumiana, karibu wauwane, hatimae Abubakr akachaguliwa.

Kama asemavyo Umar: "Kuchaguliwa kwa Abubakr kulitokea ghafla, Mwenyezi Mungu alizuia shari zake, na atakae rejesha kitendo kama hiki auliwe."

Taz. Tarikhul Tabari J.2 Uk. 446/457

Tarikh Ibn Athir J.2 Uk. 223

Sahih Bukhar J.8 Uk. 210

Albidayatu Wannihaya J.5 Uk. 215

Source URL: https://www.al-islam.org/fa/node/41274#comment-0